**Madarasa yanayoongea yalivyopunguza changamoto ya KKK Manispaa ya Songea**

**Na Albano Midelo**



MADARASA yanayoongea katika shule za msingi zilizopo Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma yamefanikiwa kupunguza changamoto ya idadi kubwa ya wanafunzi ambao walikuwa wanafika darasa la saba bila kujua Kusoma,Kuandika na kuhesabu(KKK).

Uchunguzi ambao umefanywa katika shule tatu za msingi zilizopo katika Kata za Mwengemshindo,Bombambili na Mjini umebaini kuwa tangu serikali ilipoanzisha mfumo wa madarasa yanayoongea umesababisha idadi kubwa ya wanafunzi kujua Kusoma,Kuandika na Kuhesabu tangu wakiwa katika darasa la kwanza na la pili.

Asumpta Banda ni Mwalimu ambaye anafundisha darasa la kwanza katika shule ya Msingi Tembo Mashujaa Kata ya Bombambili lenye wanafunzi 147 ambapo anasema darasa linaloongea limesababisha wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

Banda anasisitiza kuwa darasa linaloongea linawawezesha wanafunzi wake kujua (KKK) katika kipindi cha miezi mitatu na kwamba darasa linaloongea limeandaliwa kwa kuwekwa zana za kufundishia na kujifunzia ambazo zina Uwezo wa kumshawishi Mtoto kutaka kujifunza Zaidi bila hata ya uwepo wa mwalimu darasani.

“Faida kubwa ya Darasa linaloongea ni kupunguza idadi kubwa ya utoro shuleni,mwanafunzi kuwa mdadisi, mwanafunzi kuwa mbunifu,kuleta ari ya kujifunza kwa mwanafunzi na kupunguza kelele darasani”,anasema.

Mwalimu Mkuu wa shule ya Msingi Tembo mashujaa Samson Lyoba amesema kwa miaka mingi shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na changamoto ya idadi kubwa ya wanafunzi waliokuwa wanamaliza darasa saba bila kujua Kusoma,Kuandika na Kuhesabu.

Lyoba anasema mpango wa TUSOME PAMOJA ambao ulianza kutolewa mwaka 2016 kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na TAMISEMI umesababisha wanafunzi kujua Kusoma,Kuandika na Kuhesabu tangu wakiwa katika madarasa ya chini.

“ilikuwa inachukua muda mrefu kwa wanafunzi wa darasa la kwanza kujua kusoma, kuhesabu na kuandika baada ya kuanza mafunzo ya TUSOME PAMOJA Watoto wa darasa la kwanza wamekuwa wakijua haraka na kwa muda mfupi kusoma,kuhesabu na kuandika.

Ametolea mfano katika shule yake,watoto wa darasa la kwanza mwaka 2018 wapo 147 kati ya hao watoto 145 walijua kusoma,kuhesabu na kuandika kwa siku 60 na kwamba hali hiyo imetokana walimu kutumia mbinu walizopata kwenye semina ya TUSOME PAMOJA.

Hata hivyo anabainisha kuwa kabla ya TUSOME PAMOJA wanafunzi waliokuwa wanajua KKK walikuwa ni chini ya asilimia 50 na kwamba baada ya kuingia kwenye mpango huo wanafunzi wanajua KKK kwa asilimia 100.

“Darasa la kwanza lina wanafunzi 147 kati yao wanaojua KKK1 145 na wasiojua KKK ni wawili tu ambao wana matatizo ya ulemavu wa akili, katika darasa la pili pia wanafunzi wawili tu hawajui KKK wakiwa na ulemavu wa akili kwa ujumla katika shule nzima wanafunzi wanaojua KKK ni 884 na wanafunzi wasiojua KKK ni wanne”,anasema Lyoba.



Bertha Luoga ni mwalimu wa KKK katika darasa la pili shule ya Msingi Mwengemshindo lenye wanafunzi 72,anasema mpango wa TUSOME PAMOJA kwa kutumia darasa linaloongea umesaidia wanafunzi wote 70 kujua KKK tangu wakiwa darasa la kwanza na kwamba wanafunzi wawili ambao wamehamia katika shule hiyo darasa la pili ndiyo hawajui KKK.

“Mbinu ambazo zimefanikisha wanafunzi hao kujua KKK mapema ni mafunzo ambayo wameyapata walimu wanaofundisha KKK,wazazi pia wana mchango mkubwa kwa wanafunzi katika kujifunza wanaporudi nyumbani”,anasisitiza Luoga.

Anasema UWAWA na WEJ wamesaidia kwa kutembelea shule mara kwa mara pia wamekuwa wanasaidia kuwafichua watoto watoro na kuwaleta shuleni hali iliyopunguza tatizo la KKK katika shule hiyo.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa shule ya Msingi Mwengemshindo iliyopo katika Kata ya Mwengemshindo Gabriel Nyama anasema mfumo wa madarasa yanayoongea katika darasa la kwanza na la pili umesababisha idadi kubwa ya wanafunzi kujua Kusoma,Kuandika na Kuhesabu ndani ya kipindi kifupi.

Kwa mujibu wa Nyama ,darasa la kwanza katika shule hiyo, lina jumla ya wanafunzi 101 kati yao wanaojua KKK ni 77 na wasiojua KKK ni 24 ambapo darasa la pili lina jumla ya wanafunzi 72 kati yao wanaojua KKK ni 70 na wasiojua KKK ni wawili.

Shule ya Msingi Mwengemshindo ambayo ilianzishwa mwaka 1975 ina jumla ya wanafunzi 637 wakiwemo wavulana 327 na wasichana 310.Shule hiyo ina walimu 11 na vyumba vya madarasa 10.

Mratibu Elimu Kata ya Mwengemshindo Simon Kagema anasema kata hiyo ina shule mbili ambazo ni Luhirakati na Mwengemshindo, ambapo amekiri mradi wa TUSOME PAMOJA kwamba umesaidia kupunguza tatizo la KKK na utoro katika shule za Kata hiyo.

Kagema anabainisha zaidi kuwa kabla ya mradi wa TUSOME PAMOJA kuanza kulikuwa na changamoto kubwa ya utoro kwa wanafunzi wa darasa la kwanza na pili,kutokana na mlundikano wa masomo katika madarasa hayo.

Anasema mara baada ya mfumo mpya wa madarasa hayo kufundisha masomo machache ya KKK na mafunzo ambayo yametolewa kwa walimu wa madarasa hayo,maendeleo yamekuwa mazuri ikiwemo utoro kupungua kwa kiwango kikubwa.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo, kabla ya mpango huu wanafunzi katika kata yake nusu ya darasa walikuwa wanaingia darasa la pili

bila kujua KKK lakini hivi sasa kwa kutumia mpango huo karibu wanafunzi wote wanajua KKK ndani ya miezi sita.

Kagema anabainisha zaidi kuwa mdondoko na utoro wa wanafunzi katika madarasa ya kwanza na pili katika kata yake ulikuwa mkubwa miaka miwili iliyopita ukiwa ni zaidi ya asilimia 30 ambapo hivi sasa ni kati ya asilimia moja hadi mbili.

Shule ya Msingi Majimaji iliyopo katika Kata ya Mjini,ni miongoni mwa shule ambazo zimenufaika na Mpango wa TUSOME PAMOJA hali ambayo imeweza kuboresha mbinu za ujifunzaji na ufundishaji na kuondoa tatizo la KKK.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Crensensia Komba anawataja wanafunzi waliosajiriwa darasa la kwanza mwaka huu kuwa ni 105 kati yao wanaojua KKK ni 97 na wasiojua KKK ni wanafunzi wanne tu.

Amewataja wanafunzi waliosajiriwa katika darasa la pili kuwa ni 123 kati yao wanafunzi 117 wanajua KKK na wanafunzi sita hawajui KKK.

Mratibu wa Elimu Kata ya Mjini Teodory Hango anasema mradi wa TUSOME PAMOJA tangu ulipoanza kutelekezwa mwaka 2016 umeleta mafanikio makubwa katika kupunguza changamoto ya wanafunzi wasijua KKK katika madarasa ya kwanza na pili.

Anasema kata ya mjini ina shule nne ambazo ni Majimaji,St.Joseph,Mfaranyaki na Mashujaa na kwamba shule hizo zina jumla ya wanafunzi 773 wanaosoma katika madarasa ya kwanza na pili.

“Hadi kufikia Septemba mwaka huu kati ya wanafunzi hao,wanajua KKK ni wanafunzi 759 na wanafunzi wasiojua KKK ni 14,kwa mikakati ambayo tumeiweka hadi kufikia Novemba mwaka huu wanafunzi wote watakuwa wanajua KKK”,anasisitiza Hango.

Hata hivyo Hango anazitaja faida ambazo kata yake imezipata katika mradi wa TUSOME PAMOJA kuwa ni walimu wamepata stadi,ujuzi na uzoefu katika mbinu za ufundishaji wa KKK,shule

zimepata vifaa vya kujifunzia na kufundishia ambapo shule zimetoka katika uwiano wa kitabu kimoja kutumika na wanafunzi sita na kufikia kitabu kimoja kutumika kwa wanafunzi wawili.

Faida nyingine anazitaja kuwa ni ushirikiana kati ya walimu na wazazi katika kipindi cha mradi umeimarika zaidi ambapo wazazi na walezi hivi sasa wamekuwa wadau muhimu katika kujifunza na ufundishaji.

Kaimu Afisa Elimu Msingi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Sunday Wahyungi anasema Manispaa ya Songea inatekeleza mradi wa TUSOME PAMOJA kwa ushirikiano wa serikali ya Marekani kupitia Shirika la USAID na serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu na TAMISEMI.

Anasema mradi huo umeimairisha stadi za KKK katika Manispaa ya Songea na kwamba kabla ya mwaka 2016 Halmashauri ilikuwa na wastani wa wanafunzi kati ya 1300 hadi 1500 ambao walikuwa hawajui KKK wengi wao wakiwa ni darasa la pili.

Hata hivyo amesema tangu kutekelezwa kwa mradi huo,hadi kufikia Agosti mwaka huu,Manispaa ya Songea ina wanafunzi 432 ambao hawajui KKK na kwamba hadi kufikia Desemba mwaka huu wanafunzi wote hao watakuwa wanajua KKK.

“Sio kwamba wanafunzi wote hao 432 hawajui KKK kabisa,wanaufahamu ule wa kujua KKK,bali walimu bado hawajiridhisha moja kwa moja kwamba wanafunzi hao wanajua KKK kwa ufasaha”,anasisitiza.

Mkoa wa Ruvuma umejiwekea malengo ya kuhakikisha kuwa shule zote za msingi katika Mkoa ambazo ni 787 zinamaliza changamoto ya wanafunzi wasiojua KKK na kwamba ifikapo Novemba mwaka huu pasiwepo na mwanafunzi hata mmoja asiyejua KKK.

Iwapo kila shule ya msingi nchini itakuwa na darasa linaloongea lenye zana za kutosha,zinazoonekana na kusomeka Vizuri, idadi kubwa ya wanafunzi wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu nchini itapungua na hatimaye kumalizika.

**Mwandishi ni Mchangiaji wa gazeti hili mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**